

KULIFUMA KOMBE

1. Wao kulifuma kombe, sasa wanajisifia
Vichwani waota pembe, bahati wamefumia
Kama wamelewa pombe, hivyo wanavyokenua!
Kweli hatutapumua, hao kuchukua kombe
2. Mwasema nyie viwembe, nani anayewajua?
Sifa zenu ni uzembe, hilo tunawajulia
Siwapigii vijembe, ukweli naelezea
Kweli hatutapumua, nyie kuchukua kombe!
3. Ninawapeni ujumbe, watu wanavyoongea
Wawaitapo viwembe, fumbo wanawafumbia
Mzunguke kila pembe, kama mwataka fumbua
Kweli hatutapumua, nyie kuchukua kombe!
4. Wao kuchukua kombe, kweli hatutakohoa
Bado washangaa kumbe!, ndoto wanaziotea?
Kama vile ni ming'ombe, kooni wakoromea
Kweli hatutakohoa, wao kulipata kombe!
5. Mkashitaki kwa jumbe, naye atawanyakua
kuwapeleka milembe, dodoma kuugulia
Ama mtanyweshwa kombe?, kiwewe kije pungua
Pepo zimewapandia, nyie kulifuma kombe!
6. Msishutumu mjumbe, kweli kuwafikishia
Sikusaza hata chembe, wala sikuongezea
Sasa natia majembe, kazi nimemalizia
Misifa kujijazia, kisa kulifuma kombe!

*Msanif Shaban.
P.O Box 15311,
Dar es Salaam,
Tanzania. Novemba,2003*